

## **HUDUMA ZINAZOTOLEWA WODI YA WAGONJWA MAHUTUTI (ICU)**



Kuwaangalia wagonjwa kwa ukaribu zaidi ili kuwasaidia kutatua changamoto zinazojitokeza kulingana na magonjwa waliyonayo. Changamoto kati ya mgonjwa mmoja na mwingine huwa zinatofautiana hivyo hospitali imejikita katika kufanya uwangalizi wenyе umakini kulingana na changamoto mgonjwa aliyonayo.

Kuwasaidia wagonjwa ambao hawawezi kupumua vizuri kwa kuwaweka kwenye mashine za kuwasaidia kupumua na kuratibu mapigo ya moyo. Mashine hizi husaidia kuokoa maisha kwa kiasi

kikubwa kutokana na uwezo wake wa kufanya kazi. Mashine hizo ni “Mechanical Ventilator, Defibrillator na oxygen Concentrator”



kuhakikisha wagonjwa wanapata huduma stahiki ili waweze kupona haraka kama vile Kuwalisha kwa kutumia mipira, kuwapa dawa kuititia njia ya mishipa, kuwasaidia kuoga, kufanya usafi wa kinywa na kuwasaidia pia kutoa makohozi kwa kutumia vifaa maalumu.

Kuwageuza wagonjwa angalau kila baada ya saa moja ili wasipate vidonda vitokanavyo na kulala upande mmoja kwa

muda mrefu. Kufanya hivyo kunasaidia wagonjwa walioko katika wodi hiyo kuimarika haraka.

Kuwasaidia matibabu ya kisaikolojia kwa wagonjwa ambao tayari wameanza kupata ufahamu kwa kuwa wagonjwa wengi wanaoingia katika wodi hii wanakuwa wamekata tamaa au kukatiwa tamaa ya kupona.

Kuwaweka wagonjwa wote kwenye mashine za kusaidia kutambua kiwango cha oksijeni mwilini, kiwango cha upumuaji, jotoridi la mwili, shinikizo la damu na kiwango cha sukari mwilini ili kupata uhakika wa matibabu yanayotolewa.